# Vidokezo vya Upesi vya Kutumia Infinite Campus ili Kufuatilia Mwendeleo wa Mtoto wako

- **Mahudhurio:** Changanua Historia ya Mahudhurio ya Mtoto wako
  - Idadi za siku za kutokuwepo zinakaa kuwa sahihi?
  - Ikiwa unaamini kuwa kuna hitilafu:
    - Angalia tarehe ambapo mtoto wako alikuwa hayupo.
    - Ongea na mtoto wako na muulize kama alikuwepo kwenye tarehe zilizoorodheshwa.
    - Ikiwa unaamini kuwa kuna hitilafu, ipigie simu Ofisi ya mahudhurio ya shule ya mtoto wako.




- **Darasa:** Changanua Darasa za Mtoto wako
  - Gredi za mtoto wako zinakidhi matarajio ya familia yako kuhusiana na mtoto wako?
  - Ongea na mtoto wako kuhusu kila moja kati ya masomo au madarasa yake binafsi.
  - Msifu mtoto wako kwa juhudi zake na kwa kujizatiti kwake hata kama gredi sivyo vile unavyotaka ziwe.
  - Sisitiza kuwa unaamini kuwa anaweza kukidhi matarajio yako na kuwa wewe na walimu wake mko hapa ili kumsaidia apate mafanikio.




  - Ikiwa anatatizika na somo au darasa, zungumzia maswali yafuatayo unapokuwa unaangalia Lango la Mzazi:
  - **Kazi zozote za masomo zimekosekana?**
    - Ikiwa ndio, angalia tarehe kwenye kazi za masomo zilizokosekana. Mwambie mtoto ahakikishe kwa walimu wake kama anaweza kufidia kazi za masomo au kuzirudia kazi hizo za masomo.




    - Mtoto wako asipokumbuka kuwaambia walimu wake, watumie barua pepe walimu moja kwa moja au shirikiana na waajiriwa wasaidizi kwenye shule yako (Mwasiliani wa FACE, Mtetezi wa Kuhitimu wa Familia au Mwajiriwa wa Kushauri) ili kukusanya kazi za masomo zilizokosekana.
    - Mwajibishe mtoto wako akamilishe kazi zake za masomo zilizokosekana. Zingatia kutuza juhudi nyumbani ikiwa kazi za masomo zinakamilishwa na/au kuwekea kikomo manufaa hadi kazi za masomo zikamilishwe.
    - **Kidokezo: Tumia Kichupo cha Assignment na bofya "missing" kwenye sehemu ya juu ya kichupo na "Current term."**
    - Kumbuka kuwa baadhi ya kazi za masomo huenda ziwe hazikuwekewa alama kuwa ni "missing" kwa hivyo ni bora kuchanganua kila moja kati ya darasa za kazi za masomo zenye "0**".**
  - **Una matatizo kwenye Mitihani au Kwizi?**
    - Muulize kama anahitaji mawazo ya kusoma.
    - Muulize kama anapata matatizo ya kuelewa maelezo yanayojumuishwa kwenye mtihani.
    - Mhimize mtoto wako aongee na mwalimu wake kuhusu mawazo ya mazoezi ya ziada, kusoma au visaidizi vya ziada shuleni au mtandaoni.
    - Mtoto wako asipofuatilia kwa mwalimu wake, wasiliana na mwalimu moja kwa moja ili kuuliza nyenzo unazoweza kuzifikia ili kupata usaidizi wa ziada.